JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA KILIMO**

**TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA (TCDC)**

# KAMPENI YA KUIMARISHA UADILIFU NA UWAJIBIKAJI KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA

## "LINDA USHIRIKA, CHAGUA UADILIFU"

"Wanaushirika mmeanza kufanya mabadiliko muhimu yanayohitajika, ninawapongeza na endeleeni kusimamia vema maslahi mapana ya Wanaushirika."

**Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**
**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**
**Agosti 10, 2024**



**Aprili, 2026**

# KAMPENI YA KUIMARISHA UADILIFU NA UWAJIBIKAJI KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA

"LINDA USHIRIKA, CHAGUA UADILIFU"

**Aprili, 2026**

# DIBAJI

Sekta ya Ushirika ni muhimili muhimu wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini Tanzania, hususan katika kuwawezesha Wakulima, Wafugaji, Wavuvi, Wafanyabiashara na Wajasiriamali Wadogo, kupata huduma za kifedha, masoko, pembejeo na fursa mbalimbali za kiuchumi. Kupitia Vyama vya Ushirika, Wananchi wengi wameendelea kuongeza kipato chao, kujenga ustawi wa Kaya na kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa Taifa.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha Ushirika kwa kuweka na kutekeleza Sera, Sheria, Mikakati na Programu mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha Vyama vya Ushirika vinaendeshwa kwa misingi ya uadilifu, uwazi, uwajibikaji na ushiriki wa Wanachama. Hatua hizo zinalenga kuifanya sekta hii kuwa imara, shindani na yenye mchango endelevu katika pato la Taifa.

Pamoja na juhudi hizo, taarifa za Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) na ripoti za ukaguzi zinazofanywa na Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO), zimeendelea kubainisha changamoto katika uendeshaji wa Vyama vya Ushirika, zikiwemo; vitendo visivyo vya uadilifu, ubadhirifu wa rasilimali, usimamizi dhaifu wa mali, utekelezaji hafifu wa hatua za uwajibikaji, pamoja na ucheleweshwaji wa utatuzi wa migogoro. Aidha, pamoja na kuwepo kwa taarifa za Kaguzi zilipaswa kushughulikiwa na mamlaka mbalimbali, na hivyo kuchelewesha haki kwa Wanachama wa Vyama vya Ushirika na kusababisha kudhoofisha imani ya Wanaushirika, kuathiri ufanisi wa Vyama, na kuhatarisha uendelevu wa Ushirika.

Kutokana na hali hiyo, Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, imeandaa **Kampeni ya Kuimarisha Uadilifu na Uwajibikaji katika Vyama vya Ushirika,** kwa lengo la kuongeza uelewa wa Wadau kuhusu taratibu sahihi za uendeshaji na usimamizi wa Vyama vya Ushirika, kuimarisha uratibu wa Wadau wa Haki, pamoja na kuhakikisha kuwa utekelezaji madhubuti wa hatua za kisheria dhidi

ya vitendo visivyo vya uadilifu. Kampeni hii inalenga kujenga misingi imara ya uwajibikaji, haki na utawala bora katika Sekta ya Ushirika.

Utekelezaji wa Kampeni hii unatarajiwa kuchangia kufikia malengo ya kitaifa yaliyoainishwa katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya tatu (2026/27 - 2030/2031), Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 - 2050, Agenda ya Ushirika Afrika 2023 - 2033, pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030, hususan katika kukuza uchumi jumuishi, ajira na taasisi imara.

Ni matarajio yangu kuwa Wadau wote wa Sekta ya Ushirika, wakiwemo; Viongozi wa Vyama, Wanachama, Wadau wa Haki, Taasis zinazojihusisha na Ukaguzi, Vyombo vya Habari na Asasi za Kiraia, watashiriki kikamilifu katika utekelezaji wa Kampeni hii. Ushirikiano huo ni muhimu katika kulinda maslahi ya Wanachama, kuimarisha imani kwa Vyama vya Ushirika, na kuhakikisha kuwa Ushirika unakuwa chombo imara cha maendeleo ya Wananchi na Taifa kwa ujumla.

Dkt. Benson O. Ndiege
**MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA**

# YALIYOMO


DIBAJI ........................................ i

ORODHA YA VIFUPISHO ........................................ iv

1. UTANGULIZI ........................................ 1

2. UCHAMBUZI WA HALI HALISI ........................................ 2

3. MALENGO YA KAMPENI ........................................ 3

4. WADAU ........................................ 4

    4.1 Wadau Wakuu ........................................ 4

    4.2 Wadau Washirika ........................................ 8

5. MPANGO WA SHUGHULI ........................................ 5

    5.1 Uandaaji wa Nyenzo za Kutumia kwenye Kampeni ........................................ 5

    5.2 Kutoa Mafunzo ........................................ 5

    5.3 Kampeni ya Mawasiliano ........................................ 5

6. MATOKEO YANAYOTARAJIWA ........................................ 6

7. VIHATARISHI NA MKAKATI WA KUPUNGUZA ........................................ 7

8. MPANGO WA UGHARAMIAJI WA KAMPENI ........................................ 8

MAREJEO ........................................ 9

# ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **COASCO** | Co-operative Audit and Supervision Corporation *(Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika)* |
| **M&E** | Monitoring and Evaluation *(Ufuatiliaji na Tathmini)* |
| **SACCOS** | Savings and Credit Cooperative Societies *(Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo)* |
| **SMS** | Short Message Service *(Ujumbe Mfupi wa Maandishi)* |
| **TAKUKURU** | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| **TCDC** | Tanzania Cooperative Development Commission *(Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania)* |
| **TV** | Televisheni |

# 1. UTANGULIZI

Kwa mujibu wa Taarifa ya Utendaji ya Vyama vya Ushirika visivyo vya Kifedha (2023–2025), Vyama vya Ushirika vinaendelea kuwa nyenzo muhimu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Katika kipindi hicho, Vyama viliwezesha masoko ya mazao yenye uzito wa tani milioni 3.88 zenye thamani ya shilingi trilioni 6.2, hususan kupitia mazao ya Korosho, Tumbaku na Pamba. Aidha, Vyama vilisambaza pembejeo za kilimo zenye thamani ya shilingi bilioni 978, na kuchangia zaidi ya dola za Marekani milioni 124 kupitia mauzo ya nje ya Kahawa. Vilevile, Vyama vya Mifugo, Uvuvi, Madini na Ufugaji Nyuki, vimechangia katika ajira, kipato cha Wananchi na uhifadhi wa mazingira, ikiwemo upandaji wa zaidi ya miti milioni 121 (TCDC, 2025). Kwa ujumla, mchango huu unaonesha nafasi ya Ushirika kama chombo muhimu cha kukuza uchumi jumuishi, kupunguza umaskini na kutekeleza agenda za maendeleo ya Taifa.

Taarifa ya Usimamizi wa Vyama vya Ushirika mwaka 2024/25, inaonesha maendeleo makubwa katika ukuaji na uthabiti wa Vyama vya Ushirika. Kufikia mwaka 2024, Vyama vilivyokuwa vimesajiliwa ni 6,773, vikiwa na jumla ya mali zenye thamani ya shilingi trilioni 2.81.

Kwa kuzingatia mchango huo muhimu wa Vyama vya Ushirika katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii, uendelevu wa Vyama hivi unategemea kwa kiasi kikubwa mazingira ya utulivu, haki na uwajibikaji miongoni mwa Wanachama na Viongozi wao. Aidha, kumekuwepo na changamoto za Uadilifu zinazoathiri utendaji wa Vyama vya Ushirika, ikiwa ni pamoja na; ubadhirifu wa rasilimali fedha na mali, na usimamizi dhaifu wa mali za Vyama vya Ushirika. Ripoti ya jumla ya ukaguzi wa Vyama vya Ushirika kwa mwaka wa fedha 2023/24, inaonesha kuwepo kwa miamala yenye viashiria vya ubadhirifu kwa zaidi ya shilingi billioni 15.6, na mwaka 2024/25 kulikuwa na miamala yenye ubadhirifu kwa zaidi ya shilingi bilioni 14.03. Vilevile, ripoti hiyo imebainisha kuwa kulikuwa na Vyama vyenye madeni ya benki kwa muda mrefu zaidi ya shilingi bilioni 12.5, pamoja na Makampuni yanayodaiwa fedha za Wakulima kwa zaidi ya shilingi bilioni 7.4.

# 2. UCHAMBUZI WA HALI HALISI

Licha ya kuwepo kwa miongozo na mifumo ya usimamizi na uendeshaji wa shughuli za Vyama vya Ushirika, taarifa za kaguzi zinazofanywa na COASCO, pamoja na taarifa za TCDC zinaonesha changamoto zifuatazo:-

i. Ukosefu wa uwazi, uaminifu na uwajibikaji ndani ya Vyama;
ii. Bodi za Vyama kushindwa kuchukuliwa hatua kwa wakati pindi inapobainika kuwepo kwa ubadhirifu kupitia taarifa za ukaguzi, pamoja na kutokufanyia kazi mapendekezo ya ukaguzi;
iii. Uelewa mdogo wa taratibu sahihi za utatuzi wa migogoro kwa Wanachama, Viongozi na Watendaji wa Vyama vya Ushirika;
iv. Utekelezaji hafifu wa hatua za uwajibikaji, hususan Hati za Tozo kwa Viongozi na Watendaji waliosababisha hasara katika Vyama vya Ushirika;
v. Uratibu mdogo kati ya Wadau wa haki (Polisi, TAKUKURU, Ofisi ya Mashtaka, Mahakama na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali); na
vi. Mkanganyiko wa Mamlaka kati ya mifumo ya Ushirika na Mahakama katika kushughulikia migogoro baina Vyama na Wanachama/ Wadau wa Ushirika.

Athari ya changamoto hizi ni kupotea kwa rasilimali, kukosekana kwa haki za Wanachama, kupungua kwa imani ya Wanachama, Jamii na Wadau, pamoja na kuongezeka kwa migogoro na gharama za uendeshaji.



# 3. MALENGO YA KAMPENI

Lengo kuu la Kampeni hii ni kuimarisha uwajibikaji, uadilifu, na utatuzi sahihi wa migogoro katika Vyama vya Ushirika, kwa kuwahusisha Wadau wa haki.

Malengo mahsusi ni pamoja na:-

i. Kuongeza uelewa wa taratibu sahihi za uendeshaji wa Vyama, utatuzi wa migogoro inayojitokeza, na namna bora ya usimamizi wake;
ii. Kuimarisha uratibu wa Wadau wa Haki;
iii. Kuimarisha utekelezaji wa hatua za kisheria dhidi ya vitendo visivyo vya uadilifu;
iv. Kuongeza ulinzi na ufanisi wa mali za Vyama vya Ushirika nchini; na
v. Kuongeza uwajibikaji na weledi katika usimamizi na uendeshaji wa shughuli za Vyama vya Ushirika nchini.



# 4. WADAU

## 4.1 Wadau Wakuu

i. Viongozi wa Vyama vya Ushirika (Bodi na Menejimenti);
ii. Wanachama wa Vyama vya Ushirika;
iii. Wizara ya Kilimo;
iv. COASCO;
v. TCDC; na
vi. Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi.

## 4.2 Wadau Washirika

i. Wadau wa haki (Polisi, TAKUKURU, Ofisi ya Mashtaka, Mahakama na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali);
ii. Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
iii. Vyombo vya habari (TV na Redio za Kitaifa na Kijamii, Mitandao);
iv. Watoa Huduma katika Vyama vya Ushirika; na
v. Asasi za Kiraia na Mitandao ya Ushirika (kulingana na eneo husika).



# 5. MPANGO WA SHUGHULI

## 5.1 Uandaaji wa Nyenzo za Kutumia kwenye Kampeni

i. Kuandaa mwongozo kwa Wadau wa haki, unaoelezea utaratibu wa utatuzi wa migogoro;
ii. Kuandaa Andiko la hoja ya kisera ya kuanzisha Baraza la Usuluhishi kwenye Vyama vya Ushirika (Cooperative Tribunal) kama ilivyo katika baadhi ya nchi za Afrika;
iii. Kuandaa mpango wa utekelezaji wa Kampeni hii (Action plan);
iv. Kuandaa Vipeperushi, Mabango na Mwongozo mfupi wa maswali/majibu kwa Wanachama wa Vyama vya Ushirika, kuhusu utatuzi wa migogoro na uadilifu katika uendeshaji na usimamizi wa Vyama vya Ushirika; na
v. Kuandaa picha mjongeo (video clip) pamoja na vibonzo vyenye kuonesha madhara ya vitendo visivyo vya uadilifu kwenye Vyama vya Ushirika.

## 5.2 Kutoa Mafunzo

i. Mafunzo kwa Wanachama, Viongozi na Watendaji wa Vyama vya Ushirika juu ya uadilifu katika uendeshaji na usimamizi wa Vyama; na
ii. Kuwajengea uwezo Wadau wa haki (Polisi, TAKUKURU, Ofisi ya Mashtaka, Mahakama na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Wadau wengine, kama itakavyoonekana inafaa), juu ya utekelezaji wa hatua za kisheria dhidi ya vitendo visivyo vya uadilifu kwenye Vyama vya Ushirika.

## 5.3 Kampeni ya Mawasiliano

i. Vipindi vya TV;
ii. Vipindi vya Redio za Jamii na vipindi vya maswali/majibu;
iii. Jumbe mbalimbali kupitia mitandao ya kijamii; na
iv. Matukio ya Kijamii: Mikutano ya Wanachama, Maonesho, Majukwaa na Siku ya Ushirika (kulingana na kalenda ya eneo).

# 6. MATOKEO YANAYOTARAJIWA

i. Kuongezeka kwa uwazi na uwajibikaji kwenye Vyama vya Ushirika;
ii. Kushughulikia kwa wakati vitendo visivyo vya uadilifu kwenye Vyama vya Ushirika kwa kushirikiana na Wadau wa Haki;
iii. Utekelezaji wa Hati za Tozo kuimarika;
iv. Kupungua kwa ubadhilifu na vitendo visivyo vya uadilifu; na
v. Kuongezeka kwa imani ya Ushirika kwa Wanachama, Jamii na Wadau wa Ushirika.











# 7. VIHATARISHI NA MKAKATI WA KUPUNGUZA

| Kihatarishi | Namna ya kupunguza |
|---|---|
| Ushiriki mdogo wa Wadau wa haki kutokana na majukumu mengi. | kupanga vikao vifupi, ratiba rafiki, kuhusisha Viongozi wa ngazi husika mapema. |
| Taarifa finyu za migogoro na kesi za Ushirika. | Kuanzisha fomu rahisi ya ukusanyaji taarifa kwa njia ya mfumo. |
| Ukosefu wa fedha. | Kutenga fedha kwenye Bajeti ya Taasisi na kushirikisha Wadau. |
| Upinzani kutoka kwa Viongozi wasio waadilifu kwenye Vyama vya Ushirika. | Kutumia Sheria, Kanuni na Miongozo inayosimamia uendeshaji wa Vyama vya Ushirika. |



# 8. MPANGO WA UGHARAMIAJI WA KAMPENI

Ili Kampeni hii ifanikiwe vema, itahitajika raslimali fedha ya kutosha na raslimali watu, wa kusimamia utekelezaji wa Kampeni hii kwa ufanisi. TCDC kwa kushirikiana na Wizara na Wadau wa Sekta hii, watahakikisha kwamba raslimali fedha zinaratibiwa vema kwa ajili ya kufikia malengo tarajiwa.

Vyanzo vya fedha za utekelezaji wa Kampeni hii vitatokana na mapato ya ndani ya TCDC pamoja na michango toka kwa Vyama vya Ushirika na Wadau mbalimbali wa Ushirika wa ndani na nje ya nchi. Gharama halisi za utekelezaji zitabainishwa kwenye mpango kazi.



# MAREJEO

TCDC (2025). Annual Performance Report for Non-Financial Cooperative Societies, 2025. The Tanzania Cooperative Development Commission (TCDC).

TCDC (2024). SACCOS Annual Performance Report for 2024. The Tanzania Cooperative Development Commission (TCDC).

COASCO. Ripoti ya Jumla ya Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika kwa Mwaka wa Fedha 2023/24. Na 2024/25

**Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu,**
**Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania,**
Mtaa wa Kuu,
S.L.P 201,
DODOMA
**Barua pepe:** ushirika@ushirika.go.tz
**Tovuti:** www.ushirika.go.tz